ROBERT MATANO

WAZIRI wa Habari na Utangazaji Bw. Robert Matano akiapishwa kama Waziri wiki hii Ikulu ya Nairobi huku Wakuu wa shughuli za Serikali na Baraza la Mawaziri Mabw. Kierereni na Nyachae waki shuhudia.

PICHA: KNA

Waziri Ngei Aombwa Awasaidie Walamu

DIWANI wa Mji wa Kale wa Lamu, Bw. Abdul Nasir amemshukuru Rais Moi kwa hatua aliyoichukuwa juu ya swala la Maskwota kupatiwa hati za kumiliki ardhi.

Kwenye taarifa yake aliyoituma kwa *COASTWEEK*, Bw. Abdul Nasir ambaye pia ni Katibu wa chama cha Biashara tawi la Lamu alisema Rais Moi ni kiongozi anayependa kuwaona wananchi wake waikiishi kwa raha.

"Namuomba Waziri wa Ardhi na Makao, Bw. Paul Ngei ahimize afisi yake juu ya watu wa Lamu na hasa katika sehemu za Faza, Siu, Pate na kwengineko ambao wameishi katika sehemu hizo kwa miaka mingi bila ya kuwa na hati za kumiliki ardhi", akatoa ombi diwani huyo.

Bw. Abdul Nasir alisema watu kama hao hukosa mikopo kutokana na kutokuwana hati ambazo zinaweza kuwa dhamana zao na akaiomba wizara ya Ardhi na Makao iharakishe jambo hilo.

Diwani huyo alitoa pole nyingi kwa watu wa Mbajumwali ambao hivi majuzi waliteketewa na nyumba zao. Ilifahamika kuwa Mbunge wa Lamu Mashariki, Bw. Mzamil Omar alitembelea sehemu hiyo na kujionea hasara iliyowafika waliounguliwa na nyumba zao.

AHADI

Wakati huo huo, Diwani Maalum wa Baraza la Manispaa ya Mombasa, Bw. Khamis Mabee amemshukuru Waziri wa Serkali za Mitaa, Bw. Moses Mudavadi kwa kumteua kama Diwani Maalum na akaahidi kutumikia baraza hilo kwa uwezo wake.

• Diw. Khamis Mabee

Bw. Mabee alisema atashirikiana na madiwani wenzake kuona mji wa Mombasa unafanya maendeleo kudumu. "Hatuna budi kushirikiana ikiwa tutataka kuinua hali ya mji wetu", akaongeza.

Bw. Mabee alimpongeza Diwani Ahmed Shahame Mwidani pamoja na Diwani Sammuel Ndoro kwa kuchaguliwa kwao kama Meya na Meya Mdogo wa Baraza la Mombasa na akahidi kushirikiana nao.

KOCHA wa timu Harambee Stars Marshall Mulwa (Kulia) akipokea viatu vya mpira kwa timu hiyo kutoka kwa Mweka Hazina wa K.F.F. Bw. Mogaka Huku Menyekiti wa K.F.F. Bw. C. Gachanja akitazama.

PICHA: KNA

Harambee Stars . . .

SHABIKI mkubwa wa soka kutoka Likoni, Mombasa Kusini ametoa ombi kwa mashabiki wote wa kandanda pamoja na Wakenya wote kokote walipo, waiombee timu yetu ya Harambee ipate kulinyakuwa tena kombe la Challenge, *aripoti Abdulrahman Sheriff.*

Shabiki huyo, Mwalimu Hamadi Mgwisho (pichani) aliliambia *COASTWEEK* **kwamba Wakenya hawana budi kuitakia kila la heri na baraka timu yetu ya Harambee Star itakayoshiriki katika mashindano baina ya mataifa ya Afrika Mashariki na Kati.**

MASLAHI

Bw. Mgwisho ambaye pia ni Timu Meneja wa Limbe Leaf FC ya huko Likoni alisema kwamba wakati umefika kwa Wakenya kufikiria maslahi ya nchi na wasijali ama kufikiria wachezaji wametoka katika timu wanazozipenda.

MASHABIKI

"Ni jambo la kuchukiza kuna baadhi ya mashabiki wa kabumbu wanakashifu uteuzi uliofanywa. Ingawa hawakuwa na matumaini kwa vipindi vya miaka miwili iliyopita, timu yetu ilifanikiwa kuchukua kombe hilo huko Dar es Salaam, Tanzania na mjini Kampala huko Uganda". akaongeza.

Timu Meneja huyo alitoa ombi kwa nahodha mpya wa timu ya taifa, Elly Adero kuwatia moyo mkubwa wachezaji wenzake kama vile "nyani" wetu, mahmood Abbas alivyokuwa akifanya alipokuwa nahodha wa timu hiyo.

Pia alisifu uongozi wa K.F.F. kwa kumrudisha kampini Abbas na akamaliza, "tuombeni dua Harambee Stars yetu ilibakishe kombe la Challenge liwe letu la maisha".

Meya Ahmed Mwidani akihutubia karamu iliyoandaliwa na Muslim Association katika oceanic Hotel huku Waziri Mdogo wa Ardhi na Mkewe Bw. Nassir (kulia) na Meya Mdogo Diw. S. Ndoro wakisikiliza.

PICHA: CEASAR MADDANGANHA

MEYA wa Mji wa Mombasa, Diwani Ahmed Mwidani alitembelea afisi ya Kanu iliyoko Majengo mara baada ya kupewa hatamu za uongozi wa Baraza la Manispaa na madiwani wenzake. Hapa anaonekana akiwa na mwenyekiti wa Kanu wilayani Mombasa, Bw. Sheriff Nassir.

PICHA: ABEID KARAMA

Madiwani Wa Mombasa Wasifiwa Na Gandy

ALIYEKUWA Mjumbe wa Coast Advisory Council, Bwana, Abubakar Yusuf Gandy amewashukuru Madiwani wa Mji wa Mombasa kwa namna walivyoendesha uchaguzi wao kwa amani wakati walipochagua Meya mpya na naibu wa Meya na wenye viti wa kamati mbali mbali.

Bw. Gandy alivutiwa kwa nidhamu ya madiwani walipowakabidhi madaraka ya uongozi madiwani wenziwao kwa mapenzi yao bila kulazimishwa na mtu yoyote.

Bw. Gandy aliwataka madiwani wasahau tafauti zao zilizopita za kupingana, washirikiane pamoja katika kila jambo na Meya mpya pamoja na alie kuwa Meya wa zamani aliyeshindwa, Diwani Rajab Sumba.

"Madiwani wawape wananchi waliowachagua hudma bora za utumishi muhimu, kama vile usafi wa mji wetu, hali ya afya imarishwe zaidi, elimu ya watoto wetu, na kufanya uhusiano mwema kati yao kwa kuzingatia wito wa Nyayo wa Amani Upendo na Umoja ili mazao ya kazi zenu muhimu zinazotakikana na kila mwananchi zipate kufaulu", akaongeza.

Bw. Gandy vile vile alisema ni muhimu kwa Meya pamoja na viongozi waliokabidhiwa madaraka katika baraza la mji watafute kila njia ambayo itazidi kuimarisha uhusiano bora unaofaa kati ya baraza la mji na wizara inayosimamia shuhuli za mabaraza ili mipango na miradi mbali mbali ili yopangwa ya maendeleo ipate kufaulu kwa manufaa ya Taifa letu.

Amewaonya Madiwani wasikubali kabisa kuingilwa na mwanasiasa yeyote mwenye kutaka kuleta uhasama wa mzozano na kuwagawanya madiwani kwa manufaa yake binafsi na kuzorotesha maendeleo ya wananchi.

MAULIDI

WAZIRI Katika Afisi ya Rias, Bw. Hussein M. Maalim atakuwa mgeni wa heshima katika Maulidi yatakayofanyika Mokowe, wilayani Lamu, Alhamisi November 17.

Katibu wa Islahil Islamiya of Kenya, Bw. Mohammed Amana alisema Waziri atakutana na viongozi, atatoa shahada kwa wanafunzi waliofuzu na pia ataweka jiwe la msingi wa Madrassa.

Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI VYA FARUCCI KWA MSHINDI WA KWANZA NA T-SHIRT KWA WASHINDI WA PILI NA WATATU KATIKA SHINDANO JIPYA LA KUJAZA MANENO

SWAHILI CROSSWORD No. 174



KWENDA KULIA:

1. Fumbo hufumbwa mjinga mwerevu........
5. Kusafiri kwa chombo chochote.
7. Kufanya jambo kwa kujionyesha hasa jambo la dini.
8. Neno la kukataa.
9. Kama, mfano.
10. Mto wa Kenya.
11. Neno la Kukataa.
13. Mzoga.
15. Mtu ambaye si mtoto wala si" mtu mzima.
17. Ghani, tumbuiza.
18. Stesheni kati ya Mombasa Nairobi.
12. Mahali pa kwenda haja.
14. Mkuki.
16. Vuno.

KWENDA CHINI:

1. Itamu kushinda sukari.
2. ..... ndiyo mwendo.
3. .....yangu sibadili na rehani.
4. ..... haiji ila kwa ncha ya upanga.
6. Shahada ya elimu.
9. Jogoo.
11. Nusu ya neno sumu.

Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 173.

1. Fatma Shiraz (Mrs), Sanduku La Posta 85268, MOMBASA.

2. Ibrahim Tewa Faraj, Sanduku La Posta 97469, MOMBASA.

3. Suleiman K. J. Sad, Sanduku La Posta 93290, MOMBASA.

Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEK.

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO No. 173.

KWENDA KULIA

1. USHUNGU, 5. TEO, 6. ONEWA, 7. ASIA, 9. DAMJI, 12. IN, 13. KUTI, 14. MO, 15. MNO, 16. KIKUKU, 17. KAO, 18. ZEE.

KWENDA CHINI

1. UPONDO, 2. UKWAJU, 3 UTOSI, 4. BOMA, 8. INUNUE, 10. MKOKO, 11. ITIKA, 14. MIA, 16. KK.

JINA. ....

SANDUKU LA POSTA. ....

....

Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK* limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwe Muhariri *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya jumatano tarehe **Nov. 23. 1983.** saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.